

Januari 12, 2021

Familia Pendwa za Shule za Umma ya Kaunti ya Fayette:

Asante kwa kuendelea kusaidia na kuimiza watoto wenu katika majifunzo ya nyumbani wakati kesi za COVID-19 katika jamii yetu zimetuzuia kurudi darasani. Ijapokuwa inasemekana mara nyingi kwamba familia ni waalimu wa kwanza na mwalimu bora wa mtoto, mahitaji makuu yaliyowekwa juu ya familia zetu mwaka huu yamekuwa ya kushangaza. Walimu na wafanyakazi wetu wamefanya kazi ya kipekee nyakati za hali ngumu, lakini hakuna kitu kinachoweza kuchukua nafasi ya faida ya kielimu ya mafundisho ya kibinafsi.

Mpango wa FCPS wa mafundisho ya Kibinafsi una njia ya kurudi darasani. Ni zaidi kuliko kesi za kawaida za kila siku za siku moja kwa wiki, na inatuwezesha kuanza majifunzo ya kibinafsi katika eneo nyekundu za jimbo kwa kuzingatia mambo mengine, kama vile: mwenendo wa jamii, kuenea kwa taasisi, na kesi miongoni mwa wanafunzi na wafanyakazi ambazo zinaweza kupuuza zibitisho zingine.

Kwa kawaida, kesi zetu za kila siku zimekuwa zaidi ya 200 kwa siku tisa zilizopita, baada ya karibuni wiki tatu za kushuka kwa kasi. Katika siku 11 za kwanza za mwaka wa 2021, tumekuwa na wanafunzi 117 na wafanyakazi 63 wamepimwa na kupatikana na COVID-19.

Hapa ndipo tulipo:

- Tumejitolea kutekeleza mafundisho ya kibinafsi haraka iwezekanavyo.
- Kwa sasa tunatoa huduma za kibinafsi za ARC-directed kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.
- Takwimu zetu zinaonyesha tunahitaji bado kuendelea na majifunzo ya umbali wiki za Januari 19-22 na Jan. 25-29, 2021.
- Lengo letu ni kuanza hatua-kwa-hatua majifunzi ya kibinafsi mnamo wiki ya Februari 1-5, 2021. Takwimu zitaamua ikiwa huo unaweza kuwa mwanzo wa hatua kwa wanafunzi wote ambao familia zao zilichagua majifunzo ya kibinafsi au ikiwa hiyo itakuwa huduma kwa vikundi vidogo vya wanafunzi.
- Wiki ijayo, utaona mabasi yetu ya shule barabarani wakati madereva na wachunguzi wetu wanaanza kufanya mazoezi ya njia zao wakijiandaa kwa mwezi wa Februari.
- Tutaendelea kugawa chakula cha bure na kutoa msaada wa afya ya akili. Kwa maelezo zaidi tembelea www.fcps.net/gethelp.

Tumeguswa na habari za kibinafsi ambazo familia zetu nyingi zimetamka, na tunataka mujue kwamba tunashiriki kweli hamu yenu ya kurudi kwa majifunzo ya kibinafsi. Tunakaribia mwisho wa kipindi hicho cha wiki mbili na nusu baada ya likizo ambapo tunapaswa kuanza kushuka.

Hatungependa kitu chochote kingine isipokuwa kutangaza maelezo kwamba: wiki ijayo Jumanne, wiki ya kwanza ya mwezi ya Februari, ni kurudi kwa majifunzo ya kibinafsi. Kwa msaada wenu na juhudi yenu inayoendelea, tunaweza kufanikisha hilo.

Kwa dhati,

Marlene Helm

Kaimu Msimamizi wa Shule za Umma za Kaunti ya Fayette